

## GRADE 3 MID TERM 3 DECEMBER 2021

### 1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(Alama 5)

*Sikiliza hadithi nitakayokusomea kisha nitakuuliza maswali.*

Sokoni ni pahali ambapo vitu na vyakula mbalimbali huuzwa. Mtu anayeuzua bidhaa huitwa muuzaji, naye anayenunua huitwa mnunuzi. Soko letu huuzwa vitu vya aina nyingi kama mboga, viazi, mahindi, matunda na nguo. Mama yangu huenda sokoni kununua chakula.

- a) Mtu anayeuzua huitwaje? \_\_\_\_\_ (al 1)
- b) Mtu anayenunua huitwaje? \_\_\_\_\_ (al 1)
- c) Taja vitu vitatu ambavyo huuzwa sokoni kulingana na hadithi. (al 3)

\_\_\_\_\_

### 2. KUSOMA KWA SAUTI.

(Alama 10)

*Soma hadithi hii kwa sauti.*

Baba yangu ni mwanabiashara. Yeye hufanya kazi ya kuuza dukani. Baba yangu ana duka kubwa sana kwenye mji wetu. Baba yangu anajulikana sana kama mzee mwenye bidii kwani yeye anajua kuwa siri ya kufaulu ni kutia bidii kwa kuamka mapema. Yeye huamka asubuhi na mapema ili kufungua duka lake. Baba yangu huwaamkua wateja wake na kuwahudumia vizuri. Kwa sababu hiyo wateja wengi huja na kupanga foleni wakingojea kuuziwa bidhaa wanazozitaka. Kwa sababu ya bidii ya baba yangu yeye amefaulu sana na kutia fora kwenye biashara yake.